ASSEMBLIES OF GOD

EAGT

# KATIBA YA
# THE EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD
# TANZANIA

Toleo la 2011

nfinix HOT30i

CamScanner

# YALIYOMO

Contents..........................................................................................Page 01

IBARA I-Jina ..........................................................................................Page 02

IBARA YA II - Eneo la Utendaji ..........................................................................................Page 02

IBARA YA III-Makao Makuu ..........................................................................................Page 02

IBARA YA IV-Madhumuni ..........................................................................................Page 02

IBARA YA V - Misingi ya Imani ..........................................................................................Page 03

IBARA YA VI-Wadhamini ..........................................................................................Page 07

IBARA YA VII - Kamati maalum.......................................................................................... Page 08

IBARA YA VIII -Ukiri..........................................................................................Page 09

IBARA YA IX-Kuacha Utumishi..........................................................................................Page 09

IBARA YAX-Uongozi katika ngazi ya Taifa hadi Kanisa la mahali pamoja ..... Page 09

IBARAYAXI- Vikao ..........................................................................................Page 26

IBARA YA XII - Kurugenzi/Idara za Kanisa Kitaifa ..........................................................................................Page 32

IBARA YA XIII -Miradi ..........................................................................................Page 38

IBARA YA XIV - Mapato na Matumizi ya EAGT tangu Mfuko

Mkuu hadi Mfuko wa Kanisa la mahali pamoja ..........................Page 39

IBARA YA XV - Vyeti vya Watumishi ..........................................................................................Page 43

IBARA YA XVI - Muhuri wa Udhamini ..........................................................................................Page 44

IBARA YA XVII - Marekebisho ya Katiba ..........................................................................................Page 44



Infinix HOT 30i

CamScanner

# KATIBA YA
# THE EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA (EAGT)

## IBARA YA 1 - JINA

Dhehebu litajulikana kwa jina la "The Evangelist Assemblies of God -Tanzania" (E.A.G.T)

## IBARA YA II - ENEO LA UTENDAJI:

a) Dhehebu litafanya kazi katika eneo lote la Jamuhuri ya muungano wa Tanzania na litashirikiana na Makanisa mengine ya Dini yenye imani ifananayo na imani yake popote ulimwenguni na litafungua makanisa pia hata nje ya nchi.

b) Dhehebu litagawanywa katika kanda na majimbo kama itakavyoonekana inafaa na kukidhi mahitaji yake kiutekelezaji.

## IBARA YA III - MAKAO MAKUU:

Makao Makuu ya "The Evangelistic Assemblies Of God -Tanzania" (E.A.G.T) yatakuwa Dar es salaam Box 2171, Telephone Number: 022 2865171 - Dar es salaam.

## IBARA YA IV - MADHUMUNI:

1. Kutimiza agizo la Kristo (Math. 28:18-20; Mark 16:15-20; Matendo 1:8).
2. Kuanzlsha Makanisa ya mahali pamoja yanayojitegemea, yanayojiongoza, yanayojiendesha na kujieneza ambayo yanaamini, kutii na kuhubiri Injili kamili ya **YESU KRISTO.**
3. Kutoa mafunzo hai ya Kikristo kwa waumini na watu wote kwa njia ya maandiko, mafundisho ya Shule za Biblia, Kongamano (conferences), semina, mikutano ya hadhara (Crusades), Matangazo ya Redio na Television n.k
4. Kuendesha Taasisi na Idara mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza malengo yaliyotajwa.

finix HOT 30i



CamScanner

5. Kuwa na haki ya kumiliki, kushikilia kwa udhamini, kutumia, kuuza, kupanga, kupangisha, kubadilisha au vinginevyo kuachisha mali ya aina yoyote itakayoonekana inafaa kubadilisha kwa ajili ya kuendeleza kazi za E.A.G.T

## IBARA YA V - MISINGI YA IMANI:

**A. IMANI YA DHEHEBU:** Linaamini Mungu mmoja katika nafsi tatu ambaye ni Baba wa wote wamchao na ndiye aliyeumba mbingu na nchi. YESU KRISTO mwana wa Mungu ni njia pekee ya wokovu kwa mwanadamu wote. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni ahadi ya waliopokea wokovu huo.

**B. MISINGI YA IMANI: Dhehebu linaamini kuwa:**

**a) Maandiko yamevuviwa:**
Maandiko ya Agano la kale na Agano Jipya yamevuviwa kihalisi na Mungu mwenyewe na ni ufunuo wake Mungu kwa wanadamu, pia ni kiongozi cha Imani kisichoshindwa wala kubadilika (II Timotheo 3:15-17, I Wathes. 2:13; II Pet 1:21)

**b) Mungu mmoja aliye hai na wa kweli:**
Mungu mmoja tu aliye hai na aliye wa kweli amekwisha kujifunua mwenyewe kama "Mimi Niko" aliye wa milele, Muumbaji wa Mbingu na nchi na mkombozi wa ulimwengu na wanadamu. Yeye pia amejifunia zaidi kama mwenye kufuata mwenendo wa ushirikiano na uhusiano katika Baba, Mwana na Roho mtakatifu. (Kumb. 6:4, Isaya 43:10-11 na Mathayo 28:19)

**c) Uungu wa Bwana Yesu Kristo:**

Bwana Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Maandiko yanatangaza juu ya:

i. Kuzaliwa kwake na Bikira ( Math 1:18,20-25 na Lukal:31-35)

ii. Maisha yake yasiyo na dhambi (Waebr 7:26, IPet 2:22)

iii. Miujiza yake (Matendo 2:22, 10:38)

iv. Kazi yake ya malipizi juu ya msalaba (Ikor 15:3, 2kor 5:21)

v. Ufufuo wake kimwili kutika kwa wafu (Math 28:6, Luka 24:39, Ikor 15:14)

Infinix HOT 30i

CamScanner

vi. Kutukuzwa kwake upande wa kuume wa Mungu Baba ( Matendo 1:9, 11, 2:23, Wafilipi 2 : 9 -11, Ebr: sura ya 1 hadi ya 3)

## d) Anguko la Mwanadamu:

Mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu akiwa mzuri na mwema, maana Mungu alisema "Natufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu" Hata hivyo mwanadamu kwa uasi na hiari yake mwenyewe alianguka na kwa njia hiyo akajiletea si mauti ya mwili tu bali pia mauti ya kiroho ambayo ni kutengwa na Mungu (Mwanzo 1:26-27, 2:17, 3:16 na Warumi 5:12-19)

## e) Wokovu wa mwanadamu:

Tumaini la pekee la mwanadamu la ukombozi ni kwa njia ya damu ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu iliyomwagika ( Math 26:27-28, Ebr 9:22)

### i. Masharti ya Wokovu

Wokovu unapatikana kwa njia ya toba mbele za Mungu na imani katika Bwana Yesu Kristo. Kwa kuoshwa na kufanywa upya, kuzaliwa mara ya pili kwa njia ya Roho Mtakatifu na kuhesabiwa haki kwa neema kwa njia ya Imani. Mwanadamu hawezi kufanyika mrithi wa Mungu kulingana na tumaini la uzima wa milele (Luka 24:47, Yoh 3:3, Warumi 10:13, Waefeso 2:8, Tito 2:11, 3:5-7)

### ii. Ushahidi wa Wokovu

Ushahidi wa wokovu ulio wa ndani ni ule ushuhuda wa moja kwa moja wa Roho Mtakatifu (Warumi 8:16) Ushahidi wa nje kwa watu wote ni maisha ya haki na utakatifu wa kweli (Waefeso 4:24)

## f) Maagizo ya Kanisa

### i. Ubatizo katika maji mengi

Agizo la ubatizo wa kuzamisha linatolewa katika maandiko. Wote wanaotubu na kuamini Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana wanaweza kubatizwa. Kwa njia hiyo wanatangaza kwa ulimwengu kwamba wao wamekufa pamoja na Kristo na pia kwamba wao wamefufuliwa pamoja naye ili kuenenda katika upya wa uzima. (Math 28:19, Marko 16:16, Matendo 10:47-48 na Warumi 6:4)

### ii. Ushirika Mtakatifu

Meza ya Bwana itakuwa ina Mkate na Divai. ( Divai iwe maji ya matunda ya mzabibu yasiyo na mvinyo) ambayo ni mfano wa kueleza ushirika wetu wa asili ya ki-Mungu wa Bwana wetu Yeso Kristo

Infinix HOT 30i



CamScanner

kumbukumbu ya mateso yake na kifo chake hata ajapo. (Ikorintho 11:26)

**g) Ubatizo wa Roho Mtakatifu;**

Waumini wote wanatakiwa na wanayo haki ya kutafuta ahadi ya Baba; yaani ubatizo wa Roho Mtakatifu kulingana na agizo la Bwana wetu Yesu Kristo. Huu ulikuwa ni ujuzi wa kawaida kwa wale wote waliokuwemo katika kanisa la mwanzo la Kristo.

Pamoja na Ubatizo huo huja uwezo kutoka juu kwa ajiri ya maisha ya utumishi na kutolewa kwa karama pamoja na jinsi ya kuzitumia katika kazi ya huduma. (Luka 24:49, Matendo 1:4-8, Ikor 12:1-13) Ujuzi huu ni wa tofauti kabisa ingawa unalingana na ujuzi wa kuzaliwa upya. (Mndo 4:12-17, Mndo 10:44-46, 15:7-9) Pamoja na ujuzi huo wa ubatizo katika Roho Mtakatifu kunakuja ujuzi mwingine wa kujazwa mpaka kufurika kwa Roho huyo huyo. (Yoh 7:37-39); kumheshimu Mungu kwa undani zaidi (Mndo 2:42) Pamoja na upendo wenye vitendo zaidi kwa ajili ya Kristo, Neno lake na kwa ajili ya wanaopotea.

**h) Ushahidi wa ubatizo katika Roho Mtakatifu**

Ushahidi wa waumini katika Roho Mtakatifu unashuhudiwa kwa ishara ya nje iliyo ya kimwili ya kunena kwa lugha nyingine kama Roho wa Mungu anavyowajalia kutamka (Mndo 2:4). Kusema kwa lugha kunatokea wakati huu wa sasa na ni sawa na kiasi Fulani cha ile karama ya lugha (Ikor 12:4-10, 48) ingawa ni tofauti katika makusudi ya matumizi.

**i) Utakaso:**

Ni tendo la kutengwa kutokana na kile kilicho kiovu na kuwekwa wakfu ka ajili ya Mungu. (Warumi 12:1-2, IWathes 5:23, Waeb 13:12) Maandiko yanafundisha juu ya maisha ya utakatifu ambao pasipo huo hapana mtu atakayemwona Mungu (Waeb 12:14)Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu sisi tunao uwezo wa kutii amri ile. "Iweni watakatifu kama mimi nami nilivyo mtakatifu" (IPetro 1:15-16)

Utakaso huwa halisi katika mwamini kwa kugundua na kufahamu utambulisho wake na Kristo katika kifo chake na kufufuka na kwa imani akajihesabu kila mara kwamba yupo katika muungano huo, na kwa kutoa kila kiungo kila mara kwa ajili ya kutawaliwa na Roho Mtakatifu (Warumi 6:11, 13:8-12,13, Wagal 2:20, Wafilipi 2:12-13)



Infinix HOT 30i

CamScanner

**j) Kanisa:**

Kanisa ni mwili wa Kristo, Makao ya Mungu kwa njia ya Roho, lenye vyeo vya Ki-Mungu kwa ajili ya utimizo wa kazi yake kuu. Kila mwamini aliyezaliwa kwa Roho ni sehemu ya muhimu ya kanisa ambalo ni kusanyiko la wazaliwa wa kwanza ambao wameandikwa mbinguni (Waefeso 1:22-23, 2:22, na Waeb 12:23)

**k) Huduma:**

Huduma ya Ki- Mungu pamoja na utumishi uliopangwa katika maandiko umetolewa na Bwana wetu kwa makusudi mawili:

1. Kushuhudia ulimwengu
2. Kujengwa kwa mwili wa Kristo (Marko 16:15-20, Waefeso 4:11-13)

**l) Uponyaji wa Mungu:**

Uponyaji wa Mungu ni sehemu muhimu ya injili. Kufunguliwa kutokana na magonjwa ni kitu kilichopo katika malipizi na ni haki ya kila mwamini (Isaya 53:4-5, Math 8:16-17, Yakobo 5:14-16)

**m) Tumaini lenye Baraka:**

Ufufuo wa wale ambao wamelala katika Kristo ni pamoja na kunyakuliwa kwa ambao wako hai na ambao wamesalia mpaka wakati wa kuja kwa Bwana, na ndilo tumaini lenye Baraka na lililo kuu zaidi katika kanisa.(IWathes 4:14-17, Warumi 8:23, Tito 2:13)

**n) Utawala wa Kristo wa miaka elfu:**

Kuja kwa mara ya pili kwa Kristo ni pamoja na kunyakuliwa kwa watakatifu ambao ni tumaini lenye Baraka, kukifuatiwa pamoja na kurudi kwa wazi kwa Kristo pamoja na watakatifu wake kwa ajili ya kutawala hapa ulimwenguni kwa muda wa miaka elfu moja (Zek 14:5, Math 24:27-30, Ufunuo 1:7, 19:11-14, 20:1-6)

Na utawala huu wa miaka elfu moja utaleta wokovu kwa Israel kama Taifa (Ezek 37:21-22, Sefania 3:19-20,Warumi 11:26-27) Na kuanzishwa kwa amani ya ulimwengu mzima (Isaya 11:6-9, Zab 72:1-8, na Mika 4:3-4)



CamScanner

**o) Hukumu ya mwisho:**

Kutakuwepo na hukumu ya mwisho ambayo waovu wote watafufuliwa na kuhukumiwa sawasawa na matendo yao. Yeyote ambaye hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima , pamoja na shetani na malaika zake, mnyama na nabii wa uongo watateketezwa kwenye adhabu ambayo ni ya milele katika ziwa la moto liwakalo moto na kiberiti ambayo ni mauti ya pili (Math 25:46, Mark 9:43, Ufunuo 19:20, 20:11-15, 21:18)

**p) Mbingu mpya na Nchi mpya.**

Sisi kulingana na ahadi yake twatazamia mbingu mpya na nchi mpya ambamo haki inakaa ndani yake (2Petro 3:13, Ufunuo 21:22)

## WAJIBU WA UONGOZI:

Ni wajibu wa Uongozi wote wa **EAGT** kusimamia misingi ya imani ya Kanisa mahali popote ndani na nje ya Tanzania

## IBARA YA VI - WADHAMINI:

1. Balaza la Wadhamini litakuwa na wadhamini wasiopungua watatu na wasiozidi watano na litaitwa "The Registered Trustees of The Evangelistic Assemblies of God (Tanzania)".

2. Litateuliwa na Halmashauri kuu na kuthibitishwa na Mkutano mkuu.

3. Wadhamini wataomba kusajiliwa na watasajiliwa kulingana na sheria ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. Wadhamini watamchagua mwenyekiti miongoni mwao, isipokuwa Askofu Mkuu hatachaguliwa kushika nafai hiyo.

## A. SIFA ZA WADHAMINI:

1. Mdhamini ni lazima awe muumini, Mchungaji au Askofu wa Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT)



Infinix HOT 30i

CamScanner

2. Mdhamini ni lazima awe Mchungaji au Muumini wa muda mrefu na wa kutegemewa aliye mwaminifu na mkweli.

3. Mdhamini ni lazima awe na umri usiopungua miaka hamsini (50).

## B. MADARAKA NA KAZI ZA MDHAMINI

1. Wadhamini watasimamia umilikaji wa mali za EAGT kwa ukamilifu na nia njema. Kwa uangalifu na hekima kama iwapasavyo watu wa jinsi hiyo katika jamii.

2. Mali yote inayomilikiwa au itakayomilikiwa na EAGT itakuwa chini ya wadhamini kwa niaba ya EAGT.

3. Endapo wadhamini wataridhika kwa kutokana na sababu zilizopo katika Ibara ya X kifungu Na. I (c) Askofu Mkuu anapaswa kuondolewa madarakani wataipeleka agenda ya suala hilo kwenye Halmashauri kuu kujadiliwa.

4. Kikao cha Halmashauri kuu kinachojadili suala la Askofu Mkuu kwa mujibu wa Ibara ya VII kifungu Na 3. Watachagua mwenyekiti wao.

## C. KUISHA KWA WADHAMINI:

Udhamini wa Mdhamini utaisha kwa kutokana na kifo chake, kujiuzuru, kukosa uaminifu , ugonjwa wa akili au kukataliwa na Mkutano Mkuu.

## IBARA YA VII - KAMATI MAALUM

1. a) Kutakuwepo na kamati maalum

   b) Itafanya kazi kulingana na muundo wa EAGT wakati wote.

   c) Itateuliwa na Halmashauli Kuu ya EAGT

   d) Itashughulikia utekelezaji wa shughuli za Kanisa Kiserikali endapo patatokea jambo litakalokwamisha uendeshaji wa shughuli za Kanisa kwa muundo wa kawaida.

   e) Halmashauri Kuu itateua Wajumbe wasiopungua wawili kutoka kila Kanda ambayo jumla yao itakuwa kumi.



CamScanner

f) Uteuzi wa Wajumbe utadumu kwa muda wa miaka mitano.

**2. SIFA:**

Muumini, Mchungaji, Mwinjilisti au Askofu mwenye uwezo na muda wa kumudu utekelezaji wa shughuli za Kanisa Kiserikali.

## IBARA YA VIII - UKIRI

1. Mtumishi kutia saini Jimboni HATI ya UTII arnbayo itathibitishwa na Askofu wa Jimbo na katibu wa Jimbo kabla ya kukubaliwa utumishi Jimboni.

2. Mtumishi kabla ya kubarikiwa atatia saini HATI ya UTII ya kuwa mtumishi mwaminifu na mtii kwenye ngazi ya mbarikiwa. Hati hii itathibitishwa na Askofu Mkuu na Katibu Mkuu kwa kutia saini zao katika HATI.

## IBARA YA IX - KUACHA UTUMISHI

Mtumishi aachapo utumishi wake EAGT ataondoka pekee pasipo washirika wala mali za Kanisa.

## IBARA YA X - UONGOZI KATIKA NGAZI YA TAIFA EAGT HADI KANISA LA MAHALI PAMOJA

### A. NGAZI YA TAIFA

#### 1. ASKOFU MKUU:

**a) Sifa za Askofu Mkuu:**

i. Mwenye sifa zilizotajwa katika Tito 1:7-9, IPet 5:3, ITimotheo 3:1-7



Infinix HOT 30i

CamScanner

iii. Awe ametumikia EAGT kwa muda usiopungua miaka 15 kama Mwinjilisti, Mchungaji, Mwalimu au ngazi nyingine za uongozi na awe yule tu aliyebarikiwa.

## b) Kazi zake:

i. Atakuwa mmojawapo wa Wadhamini wa EAGT na ndiye mtia sahihi wa kwanza katika hati za fedha za EAGT

ii. Atakuwa mwenyekiti na kiongozi wa vikao vya Mkutano mkuu wa kawaida, Mkutano mkuu wa dharura, Halmashauri kuu, kamati ya utendaji na Mkutano mkuu wa Baraza la waangalizi.

iii. Atakuwa mwangalizi mkuu wa kusimamia na kuhakikisha kwamba kanisa linaongozwa kiroro.

iv. Ataliwakilisha kanisa katika mialiko ya sherehe na mikutano mbalimbali ya kiroho na kiserikali ndani na nje ya nchi ya Tanzania.

v. Atatumikia EAGT kwa kipindi cha miaka mitano (5) na anaweza kuchaguliwa tena na tena.

vi. Atatia saini vyeti vyote vya wachungaji wasimikwa na vya viongozi.

vii. Atashughulikia maswala ya wachungaji wote Ki-Taifa.

## c) Kuondolewa Madarakani

Askofu Mkuu atasimamishwa kwa kura za siri za maandishi kwa theluthi mblli (2/3) za wajumbe wa Halmashauri Kuu ya EAGT katika wadhifa wake kabla ya kipindi chake kumalizika kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kujiuzuru mwenyewe

ii. Kutokana na ugonjwa utakaosababisha kushindwa kulitumikia kanisa.

iii. Baada ya kuanguka dhambini na kuonekana/kubainika kuwa kuendelea kwake kuongoza kutasababisha machafuko au kama tayari amekwisha sababisha machafuko na jitihada za kumsaidia kujirekebisha zimeshindikana

Infinix HOT 30i



CamScanner

**d) Uwajibikaji:**

Askofu Mkuu atawajibika kwa Halmashauri Kuu

## 2. Makamu Askofu Mkuu

**a) Sifa zake:**

Awe na sifa sawa na zile zilizoelezwa kwa Askofu Mkuu kwenye Ibara Na. X kifungu 1 (a) (i) hadi cha (iii).

**b) Kazi zake:**

Atakaimu shughuli zote za Askofu Mkuu iwapo Askofu Mkuu atajiuzuru ghafla au atafariki au akiachishwa/akisimamishwa uongozi kabla ya kipindi chake kumalizika. Au amepatikana na hali yoyote itakayomfanya asiweze kutekeleza kazi zake kwa muda.

Pia atatekeleza shughuli zozote ambazo Askofu Mkuu atamtaka azitende kwa niaba yake.

**c) Kuondolewa Madarakani:**

Ataondolewa madarakani/kusimamishwa kwa sababu zile zile kama Ibara Na. X kifungu Na.I(c) kwa kikao cha Halmashauri kuu kitakachoitishwa na Askofu Mkuu.

**d) Uwajibikaji:**

Atawajibika kwa Askofu Mkuu.

## 3. Katibu Mkuu

**a) Sifa Zake:**

i. Mtendaji Mkuu

ii. Awe na sifa sawa na zile zilizopo katika Ibara Na. XI kifungu 1 (a) (i) na (iii).

iii. Awe mwenye umri usiopungua miaka 40.

Infinix HOT 30i

CamScanner

**b) Kazi zake:**

i. Kutunza fedha za EAGT

ii. Kutayarisha na kutunza taarifa za fedha za EAGT

iii. Mweka saini wa tatu katika hati za fedha za EAGT baada ya Katibu Mkuu.

**c) Kuondolewa:**

Mweka Hazina ataondolewa madarakani kwa sababu zile zile zilizopo katika Ibara ya X - 1 (c) au kwa sababu ya kufuja fedha au mail za EAGT.

**d) Uwajibikaji:**

Mweka Hazina mkuu atawajibika kwa Askofu Mkuu.

**5. Mkaguzi wa Mahesabu (Auditor)**

**a) Sifa zake:**

Awe Muumini au Mchungaji mwenye sifa *za* ukaguzi wa mahesabu.

**b) Kazi zake:**

i. Atakuwa Mkaguzi wa mapato na matumizi ya fedha za EAGT.

ii. Atatayarisha taarifa ya ukaguzi na kuiwakilisha kwenye vikao vya kamati ya utendaji, Halmashauri kuu na Kamati maalum inapobidi/inapolazimu.

iii. Taarifa ya Mkaguzi wa Mahesabu kamwe haitawakilishwa kwa Mweka Hazina na wala taarifa yake na ile ya mweka Hazina hazitatayarishwa kwa pamoja.

**c) Kuondolewa Madarakani**

Ataondolewa madarakani kwa hatua zile zile zilizotumika kumwondoa Askofu Mkuu, Askofu Mkuu Msaidizi, Katibu Mkuu na Mweka Hazina na kwa sababu zile zile kama ilivyo kwenye Ibara ya X - kifungu Na. 1 (c).

Infinix HOT 30i



CS CamScanner

iv. Awe ametumikia kanisa kwa muda usiopungua miaka 10 kama Mwinjilisti, Mchungaji, Mwalimu au ngazi nyingine ya Uongozi na awe aliyebarikiwa.

v. Awe Mwinjilisti, Mchungaji au Mwalimu. Endapo mtu wa namna hii atakuwa na shahada/stashahada au cheti kinachotambulika KITAIFA katika mambo ya utawala na utendaji (Administration and Management) atafaa zaidi.

vi. Atachaguliwa kama alivyochaguliwa Askofu Mkuu na Askofu Mkuu Msaidizi.

**b) Kazi zake:**

i, Mtendaji mkuu wa shughuli zote za kanisa la EAGT.

ii. Kuandaa na kuitisha mikutano ya kamati ya utendaji, Mkutano Mkuu wa kawaida, wa uchaguzi, wa dharura, wa Halmashauri Kuu na wa Baraza Kuu kwa kushauriana na Mwenyekiti (Askofu Mkuu).

iii. Kutayarisha taarifa ya utendaji na Halmashauri Kuu na kuiwakilisha katika Mkutano Mkuu.

iv. Mweka saini wa pili katika hati za fedha za kanisa la EAGT.

v. Atatia saini vyeti/vitambulisho vyote vya Watumishi waliosimikwa na vyeti/vitambulisho vya Uongozi.

**c) Kuondolewa madarakani**

Katibu mkuu ataondolewa madarakani kwa sababu zile zile zilizopo katika Ibara ya XIV, 1 (C) (i) - (iii).

**d) Uwajibikaji:**

Atawajibika kwa Askofu Mkuu

**4. Mweka Hazina Mkuu (General Transurer)**

**a) Sifa zake:**

Awe Muumini au Mchungaji mwenye sifa za uhasibu (Accountant)



inix HOT 30i

CamScanner

d) **Uwajibikaji:**

Atawajibika kwa Askofu Mkuu

## B. UONGOZI KATIKA KANDA:

a) Uchaguzi wa Viongozi wa Kanda utafanyika mara baada ya Viongozi wa Kamati Kuu ya Utendaji. Watakaochaguliwa ni:

i. Askofu wa Kanda

ii. Askofu wa Kanda Msaidizi

iii. Katibu wa Kanda

iv. Mweka Hazina wa Kanda

### b) Askofu wa Kanda

**1. Sifa zake**

i. Zitakuwa sawa na zile za Askofu Mkuu kama zilivyo kwenye Ibara ya x kifungu 1 (a) (i) na (iii)

ii. Awe na umri kuanzia miaka 40

iii. Awe ameitumikia EAGT kwa muda usiopungua miaka 10 kama Mwinjilisti, Mchungaji, Mwalimu wa shule ya Biblia au ngazi nyingineyo katika Uongozi wa EAGT na lazima awe AMEBARIKIWA.

**2. Kazi zake:**

a) Atakuwa Kiongozi na Mshauri Mkuu wa mambo ya kiroho katika Kanda yake.

b) Atatia saini vyeti/vitambulisho vyote vya Muhubiri.

c) Atatia saini ya kwanza hati zote za malipo ya EAGT katika Kanda yake

a) Atashughulikia maswala ya Wachungaji yote Ki - Kanda.



Infinix HOT 30i

CamScanner

3. **Kuondolewa Madarakani**

Ataondolewa madarakani kwa sababu zile zile zilizotajwa katika kumwondoa Askofu Mkuu kwenye Ibara ya X kifungu 1 (c) (i)-(iii). Atasimamishwa na Halmashauri Kuu na ataondolewa na Mkutano Mkuu wa Kanda.

4. **Uwajibikaji**

**Atawajibika kwa Askofu Mkuu**

c. Askofu wa Kanda Msaidizi.

1. Sifa zake:

a) Sawa na zile za Askofu Mkuu zilizopo kwenye Ibara X kifungu 1 (a) (i) na (iii).

b) Asiwe na umri chini ya miaka 40.

2. **Kazi zake**

Atakaimu shughuli zote za Askofu wa Kanda iwapo Askofu wa Kanda atajiuzuru au atafariki au akiachishwa/akisimamishwa Uongozi kabla ya kipindi chake kumalizika.

3. **Uwajibikaji:**

**Atawajibika kwa Askofu wa Kanda**

**d. Katibu wa Kanda**

1. **Sifa zake:**

a) Sawa na zile za Askofu Mkuu zilizopo kwenye Ibara X kifungu 1 (a) 0) na OH).
b) Asiwe na umri chini ya miaka thelathini na tano (35)

2. **Kazi yake**

a) Kuandaa na kuitisha mikutano ya kamati ya utendaji wa kanda na Halmashauri ya kanda kwa kushauriana na Askofu wa Kanda.



CamScanner

b) Mweka saini wa pili katika hati za fedha za malipo za kanisa la EAGT katika Kanda

c) Atatia saini vyeti/vitambulisho vya wahubiri

d) Atakuwa mwandishi na atatuma minute kwa wajumbe

**3. Uwajibikaji:**

Atawajibika kwa Askofu wa Kanda.

**e. Mweka Hazina**

**1. Sifa zake:**

a) Sawa na zile za Askofu Mkuu zilizopo kwenye Ibara X kifungu 1 (a) (i) na (iii).

b) Asiwe na umri chini ya miaka thelathini na tano (35)

**2. Kazi zake:**

a) Kutunza fedha za mfuko wa kanda

b) Kutayarisha na kutunza taarifa zote za fedha katika kanda

c) Mweka saini wa tatu katika hati zote za fedha za malipo katika kanda

**3. Uwajibikaji**

Atawajibika kwa Askofu wa kanda

**Kuondolewa madarakani:**

Askofu Msaidizi wa kanda, Katibu wa kanda na mweka Hazina wa kanda wataondolewa madarakani kwa taratibu zile zile zilizotumika kumwondoa Askofu wa kanda na kwa sababu zile zile kama ilivyo kwenye Ibara ya XIV kifungu 1 (c).

nfinix HOT 30i



CamScanner

Pia wote watachaguliwa kwa theruthi mbili (2/3) ya kura za siri za kuandika za wajumbe wa Mkutano mkuu wa Kanda.

## C. UONGOZI KATIKA JIMBO:

Kutakuwa na Viongozi wafuatao katika ngazi ya Jimbo.

i, Askofu wa Jimbo

ii. Askofu msaidizi wa Jimbo

iii. Katibu wa Jimbo

iv. Mweka Hazina

### 1. Askofu wa Jimbo:

**a)Sifa zake:**

i. Awe na sifa kama zile zilizopo kwenye Tito 1:7-9, IPetro 2:3, ITimoth 3:1-7.

ii. Awe mtu mwenye umri kuanzia miaka 30 na aliyebarikiwa.

Awe ameitumikia EAGT sio chini ya miaka 5 kama Mwinjilisti, Mchungaji au Mwalimu wa shule ya Biblia.

**b) Kazi zake:**

i. Atakuwa msimamizi na mshauri mkuu wa mambo ya kiroho katika Jimbo.

ii. Atatoa vyeti/vitambulisho kwa wachungaji/watumishi watendakazi wote waliopo jimboni.

iii. Atatia saini hati zote za malipo za fedha kwenye mfuko wa Jimbo.

iv. Atashughulikia maswala ya wachungaji na matatizo ya makanisa kwa kushauriana na Askofu msaidizi na Katibu wake.



Infinix HOT 30i

CamScanner

**c) Kuchaguliwa:**

Atachaguliwa kwa njia sawa na alivyochaguliwa Askofu wa Kanda na ataondolewa kwa njia ya kusimamishwa na Halmashauri ya Kanda na ataondolewa na Mkutano Mkuu wa Jimbo kwa sababu zile zile zilizofanya Askofu wa Kanda aondolewe.

**d) Uwajibikaji:**

Atawajibika kwa Askofu wa kanda.

## 2. Askofu wa Jimbo Msaidizi:

**a) Sifa zake:**

Awe na sifa sawa na zile zilizopo kwenye Ibara C kifungu 1 (a) (i)-(iii)

Awe mtu mwenye umri kuanzia miaka 30 na aliyebarikiwa.

**b) Kazi zake:**

Atakaimu shughuli zote za Askofu wa Jimbo endapo amejiuzuru ghafla, amefariki au ameachishwa/amesimamishwa kabla ya kipindi chake kumalizika

**c) Kuondolewa madarakani:**

Sawa na njia zilizotumika kumwondoa Askofu wa Jimbo na sababu zile zile.

**d) Uwajibikaji**

Atawajibika kwa Askofu wa Jimbo.

## 3. Katibu wa Jimbo:

**a) Sifa zake:**

i. Awe na sifa zilizopo katika Ibara X kifungu 1 (a) (i)-(iii).

nfinix HOT 30i



CamScanner

Awe mtu mwenye umri kuanzia miaka 30 na aliyebarikiwa.

**b) Kazi zake:**

i. Kuandaa na kuitisha mikutano ya Halmashauri ya Jimbo na Mkutano mkuu wa Jimbo wa kawaida kwa mashauriano na Askofu wa Jimbo.

ii. Mweka saini wa pili kwenye hati zote za malipo ya fedha kwenye mfuko wa Jimbo.

iii. Kuandika muhtasari wa vikao vyote vya Jimbo na hatimaye kutuma minutes kwa wajumbe.

**c) Kuondolewa:**

Sawa na njia zilizotumika kumwondoa Askofu wa Jimbo na sababu zile zile.

**d) Uwajibikaji:**

Atawajibika kwa Askofu wa Jimbo.

## 4. Mweka Hazina

**a) Sifa zake:**

i. Awe na sifa zilizopo katika Ibara X kifungu 1 (a) (i)-(iii).

ii. Awe mtu mwenye umri kuanzia miaka 30 na aliyebarikiwa.

**b) Kazi zake:**

i. Kutunza fedha za mfuko wa Jimbo.

ii. Kutayarisha na kutunza taarifa zote za fedha za Jimbo.

iii. Mweka saini wa tatu kwenye hati zote za malipo za fedha katika Jimbo.



Infinix HOT30i

CS CamScanner

c) Kuondolewa:

Sawa na njia zilizotumika kumwondoa Askofu wa Jimbo na sababu zili zile.

d) Uwajibikaji:

Atawajibika kwa Askofu wa Jimbo.

## D. UONGOZI NGAZI YA KANISA LA MAHALI PAMOJA.

### 1- A. MCHUNGAJI

Hii ni huduma ya kuanzisha na kusimamisha makanisa pamoja na kutangaza NENO la Mungu, Kanisa mama au mtumishi atakayeanzisha kanisa lazima kiwanja kiombwe kwa jina la "The Registered Trustees of the Evangelistic Assemblies of God Tanzania" na kuandikishwa jimboni kwa utambulisho, likiendelea kulelewa na mwanzishaji hadi hatua litakapopelekwa Jimboni. Hati hizo za viwanja ziwakilishwe kwa wadhamini kupitia Jimboni.

**a) Sifa zake:**

i. Awe ameokoka

ii. Amejazwa Roho Mtakatifu

iii. Amebatizwa katika maji mengi

iv. Awe ni mshirika mwaminifu wa EAGT

v. Awe na wito uliothibitishwa na Askofu wa Jimbo

vi. Ahitimu chuo cha Biblia cha EAGT au chuo cha TAG anapokubaliwa.

**b) Kazi zake:**

i. Ni kiongozi na mshauri wa kiroho wa Kanisa la mahala pamoja.



CamScanner

ii. Ni mwenyekiti wa vikao vyote vya kanisa la mahali pamoja

iii. Ni msimamizi mkuu wa shughuli zote za maendeleo ya kanisa

iv, Atasaini na kutoa vyeti/vitambulisho vya safari, ubatizo, kubariki watoto na vile vya Mkristo mtenda kazi

**c) Kuondolewa:**

Baada ya kushughulikiwa Ki-Biblia na kubainika hafai kuendelea na huduma, maamuzi ya mwisho yatakuwa ya Halmashauri kuu ya Jimbo.

**d) Sababu za kuondolewa:**

i. Endapo atajiuzuru

ii. Endapo atapata ugonjwa ambao utasababisha ashindwe kuhudumia kanisa. Ikiwa ugonjwa haukusababishwa na makosa, uzembe wake kanisa litawajibika kumtunza yeye na familia yake.

iii. Endapo atakwenda kinyume na misingi ya imani ya EAGT

iv. Akianguka dhambini

**e) Uwajibikaji:**

Atawajibika kwa Halmashauri kuu ya Jimbo.

## B. WAINJILISTI:

Kutakuwa na wainjilisti katika ngazi ya Kanisa,Jimbo,Kanda na Taifa

**a) Sifa zake:**

i. Sawa na zile zilizopo kwenye Ibara ya XIX kifungu I(a) (i)-(iv).

ii. Awe na wito wa Uwinjilisti ulio thibitishwa na uongozi wa ngazi inayomuhusu.



Infinix HOT 30i

CamScanner

iii. Sharti aanze na kuchunga kanisa na hata atakapoacha baadae kulichunga, Sharti awe na kanisa maalumu anapoabudu yeye na familia yake.

**b) Kazi zake:**

Kutangaza injili kwa njia ya mahubiri kanisani, mikutano ya hadhara, kongamano (conferencs) na semina

**c) Kuondolewa:**

Ataondolewa na Halmashauri kuu ya ngazi inayohusu.

**d) Sababu za kuondolewa:**

i. Endapo atajiuzuru

ii. Endapo atapata ugonjwa ambao utasababisha ashindwe kuhudumu

iii. Endapo atakwenda kinyume na misingi ya imani

iv. Akianguka dhambini

v. Kama mwinjilisti atapata ugonjwa ambao haukusababishwa na yeye mwenyewe, ofisi ya Jimbo pamoja na kanisa lake anapoabudu watawajibika kumtunza yeye na familia yake.

**e) Uwajibikaji:**

Atawajibika kwa kiongozi wa ngazi inayo muhusu

## C. UALIMU:

Kutakuwa na walimu katika ngazi ya Kanisa, Jimbo, Kanda na Taifa.

**a) Sifa zake:**

i. Sawa na zile zilizopo kwenye Ibara ya XIX kifungu 1(a) (i)-(iv)

ii. Awe na wito ulio thibitishwa na Uongozi wa ngazi inayomuhusu.

Infinix HOT 30i



CamScanner

**b) Kazi zake:**

Atafundisha neno la Mungu katika Kanisa, Semina, Kongamano na Shule za Biblia

**c) Kuondolewa:**

Ataondolewa na Uongozi wa ngazi inayomhusu

**d) Sababu za kuondolewa:**

Sawa na zile za Ibara ya XIX kifugu cha 1(d) (i)-(v)

**e) Uwajibikaji:**

Atawajibika kwa Kiongozi wa ngazi inayomhusu.

## D. MTUME (MISSIONARI)

Kutakuwa na Mitume katika ngazi ya Kanisa, Jimbo Kanda na Taifa.

**a) Sifa zake:**

i. Sawa na zile zilizopo kwenye Ibara ya XIX kifungu 1(3) (i)-(iv).

ii. Awe na wito ulio thibitishwa na uongozi wa ngazi inayomuhusu.

**b) Kazi zake:**

Atafanya kazi zinazohusu huduma yake.

**c) Kuondolewa madarakani.**

Ataondolewa na Uongozi unaomhusu

**d) Sababu za kuondolewa:**

Sawa na zile za Ibara XIX kifungu cha l(d) (i)-(v)

Infinix HOT 30i



CamScanner

**e) Uwajibikaji:**

**Atawajibika kwa Kiongozi wa ngazi inayomhusu.**

## E. WAUMINI

a) Mtu yeyote atatambuliwa kuwa ni muumini(mshirika) wa EAGT kufuatana na sifa zifuatazo:

i. Awe amezaliwa mara ya pili, Yohana 3:3-8

ii. Awe amebatizwa katika maji mengi, Mathayo 28:19

iii. Anayetoa zaka na sadaka kwa uaminifu, Malaki 3:8-10

iv. Akubaliane na misingi ya imani ya EAGT pamoja na mafundisho ya EAGT

v. Ahudhurie kwa uaminifu ibada, Ebra 10:25

vi. Aishi maisha matakatifu, IPetro 1:15-16, Ebra 12:14

b) Muumini HATATAMBULIKA kuwa muumini wa EAGT iwapo ametenda dhambi na kurudi nyuma pamoja na kukataa maonyo kutoka kwa mchungaji wake na watumishi wengine wa Mungu kufuatana na neno la Mungu kama lisemavyo katika Biblia 1 Wakori 5:9-11, Math 18:15-17, na Tito 3:10-11

**2- WAZEE WA KANISA**

a) Balaza la kanisa litatokana na miongoni mwa waumini walioteuliwa na Mchungaji na baadae kupigiwa kura za siri za kuandika na waumini, Idadi yao itategemea na uamuzi wa Mchungaji anayehusika.

**b) Sifa zao:**

Kama ilivyo katika Matendo 6:3-6, ITimoth 3:8-13

**c) Kazi zao:**

i. Kumshauri Mchungaji katika kuliongoza Kanisa



finix HOT 30i

CamScanner

ii. Kufanya kazi ya madhabahu (endapo Mchungaji hayupo au endapo amepanga wahudumie hata kama yupo)

d) Balaza la wazee limchague katibu wa kanisa ambaye atakuwa ni mwandishi wa vikao vyote vya kanisa na mtunza kumbukumbu. Pia achaguliwe mtunza hazina ambaye atatunza taarifa sahihi za mafungu ya kumi na sadaka na pia atatoa taarifa ya fedha kwenye Baraza kila baada ya miezi sita inapolazimu.

**e) Muda wa uzee wa kanisa**

Wazee wa kanisa wataongoza kwa muda wa miaka miwili (2).

f) Kuondolewa madarakani

Ataondolewa madarakani na Mchungaji baada ya kushughulikiwa ki-Biblia na kubainika hafai kuendelea na huduma

**g) Uwajibikaji:**

Watawajibika kwa Mchungaji

**3 - MASHEMASI (watumishi wa kanisa)**

a) Mashemasi watateuliwa na Mchungaji, na idadi yao itategemea na uamuzi wa mchungaji anayehusika.

**b) Sifa zao:**

Kama ilivyo katika ITimoth 3:8-13 na Matendo 6:3-6.

**c) Kazi zao:**

i. Kutumwa na mchungaji pamoja na wazee wa kanisa.

ii. Kuhesabu mapato yote ya kanisa kwa kusimamiwa na mtunza hazina wa kanisa.

iii, Kusimamia utulivu wakati wa ibada, kuelekeza wageni, waumini sehemu zao za kukaa wakati wa ibada.

**d) Muda wa ushemasi**

Watatumika muda wa miaka miwili

Infinix HOT 30i

CamScanner

**A. Kutakuwepo na Vikao vya Mikutano vifuatavyo:**

1. Mkutano Mkuu wa kawaida
2. Mkutano Mkuu wa Uchaguzi
3. Mkutano wa dharura
4. Mkutano wa Baraza la waangalizi
5. Mkutano wa Halmashauri Kuu
6. Mkutano wa Kamati ya Utendaji
7. Mikutano ya wadhamini, kanda, Jimbo, mkurugenzi/Idara

**B. MIKUTANO:**

**1. Mkutano mkuu wa kawaida:**

a) Utafanyika mara moja kila baada ya miaka miwili (2)

b) Taarifa ya Mkutano huu itatolewa siku tisini (90) kabla ya Mkutano

c) Utaudhuriwa na Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa kawaida

d) Mkutano mkuu wa kawaida ndio chombo cha juu katika maswala ya mwongozo na maamuzi ya EAGT

e) Utakuwa na kazi ya kupitisha na kurekebisha Katiba, taratibu na miongozo muhimu kuhusu kanisa

f) Utapendekeza tarehe ya Mkutano Mkuu wa Uchaguzi mwaka mmoja (1) kabla ya uchaguzi

g) Utapokea taarifa za maendeleo ya kila Kurugenzi/idara zote

h) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa kawaida ni Wachungaji wote wa EAGT wenye vyeti vya jimbo, wainjiristi wote, walimu wote wa shule za Biblia, wakurugenzi wote wa Kurugenzi/Idara na Makatibu wao, Wamisionari wote, mwenyekiti na wajumbe wote wa Kamati maalumu



Infinix HOT 30i

CamScanner

**A. Kutakuwepo na Vikao vya Mikutano vifuatavyo:**

1. Mkutano Mkuu wa kawaida
2. Mkutano Mkuu wa Uchaguzi
3. Mkutano wa dharura
4. Mkutano wa Baraza la waangalizi
5. Mkutano wa Halmashauri Kuu
6. Mkutano wa Kamati ya Utendaji
7. Mikutano ya wadhamini, kanda, Jimbo, mkurugenzi/Idara

**B. MIKUTANO:**

**1. Mkutano mkuu wa kawaida:**

a) Utafanyika mara moja kila baada ya miaka miwili (2)

b) Taarifa ya Mkutano huu itatolewa siku tisini (90) kabla ya Mkutano

c) Utaudhuriwa na Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa kawaida

d) Mkutano mkuu wa kawaida ndio chombo cha juu katika maswala ya mwongozo na maamuzi ya EAGT

e) Utakuwa na kazi ya kupitisha na kurekebisha Katiba, taratibu na miongozo muhimu kuhusu kanisa

f) Utapendekeza tarehe ya Mkutano Mkuu wa Uchaguzi mwaka mmoja (1) kabla ya uchaguzi

g) Utapokea taarifa za maendeleo ya kila Kurugenzi/idara zote

h) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa kawaida ni Wachungaji wote wa EAGT wenye vyeti vya jimbo, wainjiristi wote, walimu wote wa shule za Biblia, wakurugenzi wote wa Kurugenzi/Idara na Makatibu wao, Wamisionari wote, mwenyekiti na wajumbe wote wa Kamati maalumu



Infinix HOT 30i

CamScanner

## 2. Mkutano Mkuu wa Uchaguzi

Utakutana kila baada ya miaka mitano (5) Ili kuchagua Viongozi wafuatao: Askofu Mkuu, Askofu Mkuu Msaidizi, Katibu Mkuu, Mweka Hazina Mkuu, Mshauri Mkuu na Wadhamini wa EAGT.

a) Utachagua Mweyekiti na Katibu wa muda ambao wataendesha Mkutano hadi Askofu Mkuu na Katibu Mkuu watakapochaguliwa.

b) Uchaguzi utafanyika kwa kura za siri za kuandika

c) Viongozi watachaguliwa kwa theluthi mbili (2/3) za kura za siri za kuandika za Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi.

d) Endapo utaratibu wa kifungu (c) umeshindikana mara tatu mfululizo, basi kura ya zaidi ya nusu za Wajumbe wote zitahitajika ili kupitisha maamuzi.

e) Endapo utaratibu wa kifungu (c) na (d) hapo juu basi mwenyekiti atapiga kura yake.

## 3. Mkutano Mkuu wa dharura:

Mkutano Mkuu wa dharura utaitishwa kwa dharura ikilazimu ili kujadili kutafiti maswala maalum.

## 4. Mkutano wa Baraza la Waangalizi:

a) Utakuwa na Wajumbe wafuatao:

Askofu Mkuu, Askofu Mkuu Msaidizi, Katibu Mkuu, Mtunza Hazina Mkuu, Mshauri Mkuu, Wadhamini, Maaskofu wa Kanda, Makatibu wa Kanda, Maaskofu wasaidizi wa Kanda, Watunza Hazina wa Kanda, Maaskofu wa Majimbo, Makatibu wa Majimbo, Maaskofu wasaidizi wa Majimbo, Watunza Hazina wa Majimbo, Wakurugenzi wote na Mwenyekiti wa Wamissionari.

b) Utakuwa mara moja kwa mwaka

c) Taarifa ya Mkutano huu itatolewa siku sitini (60) kabla ya kikao

d) Utaandaa mipango na taratibu za Mkutano Mkuu

Infinix HOT 30i

CamScanner

e) Utapokea na kujadiii taarifa mbalimbali za kurugenzi/idara, Kanda na majimbo

f) Utakata mashauri ya watumishi na wachungaji

**5 Mkutano wa Halmashauri Kuu:**

a) Halmashauri Kuu itakuwa na wajumbe wafuatao: Wadhamini, wajumbe wote wa kamati ya utendaji, Maaskofu wa Kanda, Makatibu wa Kanda, Watunza Hazina wa Kanda, Maaskofu wasaidizi wa Kanda, Mwenyekiti wa wamissionari na Wakurugenzi wote

b) Utapokea ajenda toka kwenye Kanda kwa ajili ya Mkutano Mkuu (General conference).

c) Utapokea majina ya wadhamini, Wakurugenzi na Makatibu wa Kurugenzi/Idara zote na kupeleka kwenye mkutano wa uchaguzi au mikutano mikuu ya Kurugenzi/Idara ili kupigiwa kura za siri za maandishi na wajumbe.

d) Utakuwa na uwezo wa kuunda kamati ndogo ndogo kwa utekelezaji wa mambo ya dharura.

e) Utawakilisha mapendekezo yake, maoni na uteuzi kwa kamati ya utendaji kwa ajili ya utekelezaji ipasavyo.

f) Utakutana kila mwaka mara moja au mara mbili ikibidi.

g) Utaunda kamati za kurugenzi za kanisa ambazo kazi zake ni kukuza huduma mbalimbali katika EAGT.

h) Utapokea agenda toka kwa wadhamini kwa mujibu wa Ibara ya VIII kifungu cha tatu.

**6. Mkutano wa kamati ya Utendaji:**

a) Kamati ya Utendaji itakuwa na wajumbe wafuatao: Askofu Mkuu, Askofu Mkuu Msaidizi, Katibu Mkuu, Mweka Hazina Mkuu.



Infinix HOT 30i

CamScanner

b) Utakutana kila mwaka kupanga na kukisia gharama za uendeshaji Makao Makuu na shughuli zake na utakutana pia mara kwa mara pindi inapoitajika.

c) Utaandaa agenda za mkutano wa Halmashauri kuu pamoja na kuandaa mkutano wa Halmashauri Kuu.

d) Utasimamia kazi na kutathimini taarifa zote za maendeleo na utekelezaji wake kama zilivyopendekezwa na Halmashauri Kuu

e) Utasimamia uchaguzi wa Viongozi wa Kanda

7. Mikutano ya Bodi ya wadhamini itafanyika kabla ya mkutano mkuu wa kawaida na inapobidi wakati wowote kabla ya vikao vingine vya Kitaifa

## 8. Mikutano ya Kanda na ya Jimbo

### a) Vikao vya Kanda

i. Mikutano mikuu ya Kanda itafanyika kila baada ya miezi sita kwa madhumuni ya kutekeleza shughuli za kanda na uongozi wa kanda.

ii. Wajumbe wake ni: Askofu wa Kanda, Katibu wa Kanda, Askofu msaidizi wa Kanda, Mtunza Hazina wa Kanda, Maaskofu wote wa majimbo katika Kanda na wasaidizi wao, Makatibu wamajimbo na watunza Hazina wote wa majimbo hayo, wachungaji wote na wainjilisti katika Kanda.

### b) Kamati kuu ya Kanda

Kamati ya utendaji ya kanda itakuwa na wajumbe wafuatao: Askofu wa Kanda, Katibu wa Kanda, Askofu msaidizi wa Kanda, Mtunza Hazina wa kanda.

### c) Kazi yake:

i. Kusimamia utekelezaji wa mipango na maazimio ya Halmashauri ya kanda.

ii. Kuandaa mipango ya mikutano ya Halmashauri ya kanda

Infinix HOT 30i



CamScanner

## 1 Mkutano Mkuu wa Jimbo

### a) Kazi zake

i. Mkutano Mkuu wa kawaida utafanyika kila baada ya miezi minne

ii. Utajadili maendeleo ya kazi ya Mungu Jimboni.

iii. Utapokea taarifa za kazi toka kila Kanisa

iv. Kupokea taarifa za kazi kutoka kwa Wakuu wa Kurugenzi/Idara zilizopo Jimboni

v. Kupokea Wachungaji na Wainjilisti wapya Jimbo.

### b) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo ni:

i. Askofu wa Jimbo (Mwenyekiti)

ii. Katibu wa Jimbo, Mtunza Hazina, Askofu wa Jimbo Msaidizi, Wachungaji na Wainjilisti wote waliopo Jimboni, Wakuu wa Idara, Waalimu na Wamissionari waliopo Jimboni.

## 2. Mkutano Mkuu wa Uchaguzi:

a) Utafanyika kila baada ya miaka mitano (5)

b) Kazi yake ni kuchagua Viongozi wa Jimbo

## 3. Halmashauri Kuu ya Jimbo:

### a) Wajumbe wake:

i. Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji wa Jimbo

ii. Wachungaji wote wa Makanisa Jimboni waliobarikiwa

Infinix HOT 30i

CamScanner

**d) Halmashauri Kuu ya Kanda**

I. **Wajumbe wake**

Wajumbe wote wa Kamati Kuu ya Kanda, Maaskofu wote wa Majimbo katika Kanda, Makatibu wote wa Majimbo katika Kanda, Maaskofu wote wasaidizi wa Majimbo katika Kanda na watunza hazina wote wa Majimbo katika Kanda

ii. **Kazi yake:**

a) Kupanga na kujadili maendeleo ya kazi katika Kanda

b) Kuwapokea na kuwathibitisha watumishi, wachungaji katika kanda

c) Kuthibitisha na kuwasilisha majina ya wachungaji wanaostahili vyeti vya MHUBIRI na MSIMIKWA kwenye kamati kuu ya utendaji

d) Kupokea na kujadili agenda zitakazopelekwa kwenye mkutano wa Baraza Kuu la Waangalizi

e) Itashauri na kusuruhisha matatizo ya watumishi na wachungaji katika Kanda

f) Itakutana mara moja kila mwaka

**C - VIKAO VYA JIMBO:**

**Kutakuwa na vikao vifuatavyo katikaJimbo:**

I. Mkutano mkuu wa kawaida

II. Mkutano Mkuu wa Uchaguzi

III. Halmashauri Kuu

IV. Kamati ya utendaji



nfinix HOT 30i
CamScanner

**a) Idara ya utawala wajumbe wake ni:**

i. Askofu Mkuu

ii. Katibu Mkuu

iii. Mweka Hazina Mkuu

iv. Wadhamini wawili (2)

v. Maaskofu wote wa Kanda

**b) Idara ya Udhamini itakuwa na Wajumbe wafuatao:**

i. Askofu Mkuu

ii. Katibu Mkuu

iii. Mweka Hazina Mkuu

iv. Wadhamini wawili (2)

v. Umishenari wa Nchi husika

**c) Kazi:**

**a) Idara ya Utawala:**

i. Itaangalia imani ya kanisa ni moja katika nchi zote kanisa linapoanzishwa kwa umisheni

ii. Kutoa madaraka kwa mwenye wito kuanzisha kanisa kwenye Nchi yeyote

iii. Kumtia moyo mmishenari kusimamia kwa uwezo wote madhumuni makuu ya Kanisa ambayo ni:

- Kujitegemea
- Kujiongoza
- Kujiendesha
- Kujieneza

Infinix HOT 30i

CamScanner

**b) Idara ya Udhamini**

i. Kudhamini mali yote ya Bodi ya Umisheni kwa uaminifu, uangalifu na hekima yote.

ii. Mali zote zisizohamishika na zile zinazohamishika za Bodi ya Umisheni zitakuwa chini ya wadhamini kwa dhamana

## 2 - KURUGENZI/IDARA YA C.G.M. (Christ Gospel Messenger)

i. Itaongozwa na Mkurugenzi wa C.G.M

ii. Mkurugenzi wa CGM lazima awe ni Mchungaji na awe tu Yule aliyebarikiwa

iii. Ataongoza kwa kipindi cha miaka mitano (5)

iv. Wajumbe wa kamati ya Utendaji watakuwa ni Mkurugenzi, Katibu na mtunza Hazina

**a) Wajibu wa Kurugenzi**

**Wajibu wa Kurugenzi/idara hii ni:**

i. Kusaidia vijana kwa njia ya mafundisho ili wakue katika hali ya kumcha Mungu

ii. Kuwasaidia vijana kusudi wajue jinsi ya kumtumikia Mungu kwa njia ya kushuhudia Neno la Mungu mitaani, sokoni, hospitalini, magerezani, mashuleni, mikutano ya hadhara na ushuhuda wa nyumba kwa nyumba

iii. Kuwasaidia vijana ili wajue jinsi ya kutegemeza makanisa na shule za Biblia

iv. Kuwaandaa vijana kwa ajili ya utumishi mbeleni

**b) Mikutano ya C.G.M**

Christ Gospel Messenger watakuwa na mikutano ifuatayo:

i. Mkutano mkuu wa uchaguzi ambao utafanyika kila baada ya miaka (5) ili kuwachagua viongozi wa Kitaifa wafuatao:



Infinix HOT 30i

CamScanner

4. **Kamati ya Utendaji ya Jimbo:**

a) **Wajumbe wake:**

Askofu wa Jimbo, Katibu, Askofu Msaidizi wa Jimbo na mweka Hazina

b) **Kazi yake:**

i. Kusimamia utekelezaji wa mipango na maazimio ya Halmashauri ya Jimbo
ii. Kuandaa mipango ya mikutano ya Halmashauri kuu ya Jimbo na mkutano rnkuu wa Jimbo

## IBARA YA XII - KURUGENZI/IDARA ZA KANISA KITAIFA

Kutakuwa na kurugenzi/idara zifuatazo:

a) Bodi ya Umisheni

b) C.G.M (Christ Gospel Messenger) Wajumbe wa Yesu Kristo wa Injili

c) W.W.I (Wanawake wa Injili)

d) Kwaya

e) Elimu na Mafunzo

f) TEBE

### 1 - Bodi ya Umisheni

Bodi ya umisheni itakuwa na Idara mbili (2)

i. Idara ya Utawala

ii. Idara ya Udhamini



CamScanner

a) Mkurugenzi

b) Mkurugenzi msaidizi

c) Katibu

d) Mweka Hazina

ii. Mkutano mkuu wa kawaida ambao utakutana kila mwaka mara moja ili kutoa taarifa za kazi kwa mwaka. Kuidhinisha mapato na matumizi ya kurugenzi/idara kwa mwaka, kuweka malengo ya mwaka ujao, pia kupata maoni/mapendekezo ya kurekebisha muundo/kanuni za idara.

Kuendesha semina na mafunzo kwa ajili ya viongozi na wanachama wa idara. Kupokea taarifa toka kanda na majimbo. Mikutano yote sharti itolewe taarifa ya mwito wa miezi mitatu kwa wajumbe.

iii. Kutakuwa na Mikutano ya Kanda na Majimbo ambayo mikutano yake sharti ifuate utaratibu wa Kitaifa.

iv. Wakurugenzi wote wa Idara/Kurugenzi kuanzia ngazi ya Taifa hadi kwenye Majimbo sharti wawe wameoa na wawe na sifa za Biblia Tito 2:3-5.

## 3 - Kurugenzi ya W.W.I (Wanawake wa Injili)

### a) Wajibu wa kurugenzi hii ni:

i. Kuwaunganisha wakina mama wa Nchi nzima katika kumtumikia Mungu katika kueneza injili, kutegemeza Makanisa kutegemeza Shule za Biblia

ii. Kusaidiana wao kwa wao katika mambo mbalimbali yanayohusu unyumba (Ndoa ya Kikristo)

iii. Kuwasaidia wasichana na watoto kiroho, pamoja na huduma nyingine watakazowajibika kusaidiana katika kanisa ambazo zitaliletea kanisa Baraka.

### b) Mikutano ya W.W.I

Wanawake wa Injili watakuwa na Mikutano ifuatayo:

Infinix HOT 30i



CamScanner

Mkutano mkuu wa Uchaguzi ambao utafanyika mara moja kila baada ya miaka mitano (5) ili kuchagua Viongozi wa Kitaifa ambao ni:

a. Mkurugenzi wa W.W.I

b. Mkurugenzi msaidizi wa W.W.I

c. Katibu

d. Mweka Hazina

Mkutano mkuu wa kawaida utafanyika kila mwaka mara moja ili:

a. Kutoa taarifa za kazi za mwaka mzima

b. Kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya idara kwa mwaka unaofuata

c. Kushughulikia matatizo yote yaliyopo kwenye Idara

d. Kupokea taarifa toka kwenye Majimbo na Kanda

e. Kupokea maoni yanayohusu kurekebishwa kwa muundo/kanuni za W.W.I

f. Kuendesha semina na mafunzo kwa ajiri ya viongozi na wanachama wa idara

g. Taarifa ya vikao vyote hivi itolewe miezi mitatu kabla ya siku ya kikao kwa maandishi.

h. Mkurugenzi wa Idara hii sharti awe mwanamke aliyeolewa au aliyekwisha olewa na mumewe akafariki na awe na sifa za Biblia Tito 2:3-5 na awe na umri usiopungua miaka 35.

Mikutano ya Kanda na Majimbo chini ya Idara hii itafuata utaratibu wa Kitaifa katika kuchagua Viongozi wake na shughuli za kufanya

**4 - Kurugenzi ya kwaya:**

a) Wajibu wa kurugenzi hii ni:

nfinix HOT 30i



CamScanner

i. Kukuza huduma ya uimbaji Makanisani kwa ajili ya kutangaza / kuhubiri injili kwa njia ya nyimbo.

ii. Kusaidia kuinua kiwango cha huduma ya walimu katika Makanisa ya EAGT kwa njia ya kupata mafundisho / semina kuhusu uimbaji.

b) Kurugenzi / idara ya kwaya itaongozwa na Mkurugenzi wa kwaya aliyechaguliwa. Mkurugenzi aliyechaguliwa sharti awe na ujuzi wa kusoni note na kupiga / kutumia vyombo mbalimbali vya muziki.

c) Itakutana kila mwaka mara moja ili:

i. Kupokea taarifa toka kwenye kanda na majimbo kuhusu kwaya.

ii. Kuendesha semina/mafundisho kwa ajili ya viongozi na wanachama wa idara

iii. Kuandaa na kupendekeza majina ya waimbaji watakaofaa kwa ajili ya mafunzo ya kuendesha idara

iv. Taarifa ya kuitisha kikao itolewe miezi mitatu kabla ya kikao kwa maandishi.

d) Idara itakuwa na Mkutano Mkuu wa uchaguzi utakaofanyika kila baada ya miaka (5) ili kumchagua

i. Mkurugenzi

ii. Mkurugenzi msaidizi

iii. Katibu

iv. Mweka Hazina

e) Mikutano mingine ya kanda na majimbo itafuata taratibu za idara hii za Kitalfa

### 5 - Kurugenzi ya Elimu ya Mafunzo (Mission)

Wajibu wa kurugenzi hii ni:

Infinix HOT 30i



CamScanner

i. Kuendesha huduma ya maandiko na utayarishaji, uchapaji, ugawaji na uuzaji wa vitabu vyenye maandiko matakatifu kwa ajili ya shule ya jumapili, Tracts na maduka ya vitabu.

ii. Ihusike na uanzishaji, ujenzi na uendeshaji wa shule za Biblia, shule za mafunzo ya kawaida, studio ya kutoa mafundisho au kutangaza neno la Mungu

**6 - Kurugenzi ya TEBE (The Evangelistic Board of Evangelism)**

a) Itaongozwa na Mkurugenzi ambaye ni Mchungaji aliyebarikiwa

i. Ataongoza kwa muda wa miaka mitano (5)

ii. Wajumbe wa kamati ya utendaji ni:

- Mkurugenzi
- Katibu
- Mtunza Hazina

b) Wajibu wa Kurugenzi ni kuhubiri injiri ndani na nje ya nchi.

c) Kutakuwa na uchaguzi kila baada ya miaka mitano (5) kuchagua wajumbe wafuatao:

i. Mkurugenzi

ii. Katibu

iii. Mtunza Hazina

## IBARA YA XIII - MIRADI:

1: Dhehebu la EAGT litaendesha miradi nchini chini ya sheria za uendeshaji biashara Kama vile, maduka, viwanda vidogo vidogo, usafirishaji, shule, hospitali, zahanati hoteli, hosteli n.k

**2: Madhumuni ya kuendesha miradi:**

a) Kusaidia gharama za ujenzi wa majengo mbalimbali ya EAGT.

a) Kusaidia kulipa mishahara ya wafanyakazi



CamScanner

ii. Mafungu ya kumi ya wajumbe wote wa Halmashauri kuu

iii. Zaka za walimu na wainjilisti wa ngazi ya Kitaifa

iv. Zaka ya zaka ya wachungaji wote Jimboni

v. Sadaka na michango

vi. Miradi ya EAGT ya Kitaifa

vii. Misaada toka kwa wadhamini mbalimbali.

g) Fedha zote ziwekwe Benki na malipo yote yafanywe kwa hundi au cash. Askofu Mkuu, Katibu Mkuu na Mweka Hazina ndiyo watia saini kwenye hati zote za malipo

**2 - Mfuko wa Udhamini:**

a) Kutakuwa na Mfuko wa Udhamini ambao mapato yake yatatokana na Mfuko Mkuu kutoa robo (1/4) ya mapato yake kwenye Mfuko huu pamoja na zaka za viongozi wote wa kamati kuu ya utendaji ya EAGT

b) Utatumika kugharamia safari za Wadhamini pamoja na malipo mbalimbali

**3 - Mfuko wa Kanda**

a) Kutakuwa na mfuko wa Kanda utakaoitwa “Zonal Fund”

b) Mtunza Hazina atatakiwa kutoa stakabadhi kwa kila mapokeo ya fedha

c) Fedha hii itatumika kugharamia safari za Viongozi wa kamati kuu ya utendaji ya Kanda na kulipia gharama za ofisi.

d) Mapato ya mfuko huu yatatokana na:

i. Mapato ya mfuko huu yanatokana na Asilimia ishirini (20%) ya zaka zote toka makanisa yote yaliyopo jimboni.



Infinix HOT 30i

CamScanner

c) Kugharamia mafunzo kwa waumini na watumishi wa EAGT

d) Kulipia ununuzi wa vifaa vya ofisi

e) Kusaidia maendeleo ya jamii kwa ujumla au kazi nyinginezo.

## IBARA YA XIV - MAPATO NA MATUMIZI YA EAGT TANGU MFUKO MKUU HADI MFUKO WA KANISA LA MAHALA PAMOJA:

### 1. Mfuko Mkuu

a) Kutakuwa na mfuko mkuu wa fedha utakaojulikana kama Mfuko Mkuu (Central Fund) wa EAGT

b) Mtunza Hazina wa Mfuko huu atatakiwa kutoa stakabadhi kwa mapokeo yote ya fedha

c) Fedha hii itatolewa kwa ajiri ya posho ya Viongozi wa Kamati Kuu ya utendaji kila mwezi, kulipia gharama za ofisi, kulipia mishahara ya wafanyakazi walioajiriwa Kitaifa, matengenezo ya vyombo na mali za EAGT pamoja na kugharamia safari za Viongozi wa Kamati Kuu ya Utendaji. Halmashauri Kuu ndiyo itatoa mwongozo wa matumizi ya Mfuko Mkuu.

d) Kutunza yatima na wajane wa wachungaji na wa ongozi wa Kitaifa.

e) Hatima ya Viongozi waliotajwa hapo chini, baada ya kushindwa kutumika EAGT itawatunza hadi kifo ilimradi wanadumu kwenye imani ya EAGT. Hii ni pamoja na wake zao:

1. Rev. Moses Kulola
2. Rev. Asumwisye Mwaisabila
3. Rev. Anyandwize Mwakisyala
4. Mke wa marehemu Mamwenda
5. Rev. John H.F Mfuko

f) Mapato ya mfuko huu yatatokana na:

i. Mafungu ya kumi ya mapato ya kila kanisa

Infinix HOT 30i



CamScanner

ii. Mafungu ya kumi ya Maaskofu wote wa Majimbo katika kanda ile, Makatibu wa Majimbo, Maaskofu wasaidizi wote wa Majimbo na watunza Hazina wote wa majimbo katika kanda ile.

iii. Sadaka na michango

iv. Zaka zote za Wainjiristi na Walimu wa ngazi ya Kanda

e) Feza zote ziwekwe Benki na malipo yote yafanywe kwa hundi au cash

f) Askofu wa Kanda, Katibu wa Kanda na Mtunza Hazina wa Kanda ndiyo watia saini kwenye hati zote za malipo ya fedha.

**4-Mfuko wa Jimbo:**

a) Kutakuwa na mfuko Mkuu wa Jimbo ambao utajulikana kama "Regional Fund"

b) Mtunza Hazina atatakiwa kutoa stakabadhi kwa kila mapokeo ya fedha atakazopokea

c) Mapato ya mfuko huu yatatokana na Mafungu (zaka) ya kumi ya Wachungaji walio Jimboni. Sadaka maalumu na michango, misaada toka kwa wafadhili au miradi ya Jimbo

d) Fedha za Jimbo zitatumika kuwasafirisha wajumbe wa kamati ya utendaji wa Jimbo. Kulipa gharama za ofisi pamoja na kutengeneza vyombo na mali ya EAGT Jimboni.

e) Vitabu vya Fedha vitakuwa wazi kwa ajili ya kukaguliwa na mkaguzi wa kitaifa ikiwa lazima.

**5 - Mfuko wa Kanisa la Mahali Pamoja:**

**a) Mapato ya mfuko huu yatatokana na:**

i. Sadaka
ii. Zaka itokanayo na 10% ya pato la kila mshiriki katika kanisa la mahali pamoja ambayo yote ni ya Mchungaji.

Infinix HOT 30i



CamScanner

iii. Miradi ya kanisa la mahali pamoja
iv. Michango
v. Misaada toka kwa wafadhili.

**b) Matumizi ya Mfuko huu ni:**

i. Asilimia kumi (zaka) ya mapato, baada ya kutolewa asilimia ishirini (20%) toka zaka itapelekwa kanda. Asilimia salia itapelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa EAGT. Michango ya misaada toka kwa wafadhili haitakatwa chochote ni kwa ajili ya matumizi ya kanisa la mahali pamoja.

ii. Kulipia ghalama za ofisi kama umeme, maji na simu

iii. Chakula cha wageni wa kanisa

iv. Ujenzi wa kanisa na nyumba ya Mchungaji

v. Kulipia safari za Mchungaji anaposafiri kwenda kwenye mikutano ya Jimbo, Kanda na Taifa

vi. Matumizi mengine kama Baraza la wazee na Mchungaji watakavyoamua

vii. Baada ya Mchungaji kutumika katika kanisa moja kwa muda usiopungua miaka kumi na kanisa lina waumini wasiopungua arobaini ambao wana kipato cha kuridhisha, Kanisa hilo limjengee Mchungaji nyumba yake ya binafsi kwa maisha yake ya baadaye.

viii. Endapo kanisa litakuwa na waumini pungufu ya arobaini lakini wenye kipato cha kuridhisha watapaswa pia kumjengea Mchungaji nyumba yake ya Binafsi.

c) Fedha zote zipelekwe Benki na malipo yote yafanyike kwa hundi au cash

d) Makanisa ambayo ni machanga, Mchungani apewe posho yake toka kwenye mapato yote ya kanisa mpaka kanisa litakapokomaa.

e) Wawekaji saini kwenye Account ya kanisa wawe ni:

   i. Mchungaji saini ya kwanza na ya lazima katika kila hati na hundi za malipo.



ix HOT 30i

CamScanner

ii. Mtunza Hazina wa Kanisa

iii. Katibu wa Kanisa.

## IBARA YA XV - VYETI VYA WATUMISHI:

**Kutakuwa na vyeti vya watumishi vya aina zifuatazo:**

i. **Vyeti vya Uongozi**
Vitatolewa kwa Viongozi wa kanisa wa ngazi zote tangu Taifa hadi Jimbo, na Mtumishi atakapoondoka kwenye Uongozi lazima arudishe Cheti hiki kwa katibu Mkuu.

ii. **Vyeti vya Msimikwa** - Vitatolewa kwa Mchungaji **aliyebarikiwa tu.**

iii. **Vyeti vya Mhubiri**
Vitatolewa kwa Mtumishi ambaye hajabarikiwa lakini aliye na wito tayari uliothibitishwa na Halmashauri Kuu ya Jimbo

iv. **Vyeti vya Mtumishi Mtendaji** - Vitatolewa na Askofu wa Jimbo

v. **Vyeti vya Mkristo Mtendakazi**
Vitatolewa kwa Wakristo watenda kazi tu na Mchungaji wao

vi. **Vyeti vya Safari**
Vitatolewa na Mchungaji kwa Mkristo anayesafiri / anayehama toka Kanisa moja kwenda sehemu nyingine / Kanisa lingine

vii. **Vyeti vya Ubatizo**
Vitatolewa na Mchungaji kwa wale wote waliobatizwa baada ya Kumkiri Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao.

viii. **Vyeti vya Kubariki Watoto**
Vitatolewa na Mchungaji kwa watoto wote walioletwa kanisani na kuwekwa wakfu kwa Bwana

ix. **Vyeti vya wake wa Wachungaji**
Vitatolewa na Askofu wa Kanda kwa wake wa wachungaji

x. Kamati ya Hati itakuwa ni Kamati Kuu ya utendaji ya EAGT ambayo itatengeneza vyeti vya aina zote na kuvigawa kwa Viongozi wanaohusika kwa mujibu wa katiba.

Infinix HOT 30i



CamScanner

## IBARA YA XVI - MHURI WA UDHAMINI:

i. Mhuri utakaotumika kwenye hati utakuwa na jina la "THE REGISTERED TRUSTEES OF THE EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA"

ii. Mhuri utawekwa kwenye Hati kuthibitishwa na angalau wadhamini wawili.

## IBARA YA XVII - MAREKEBISHO YA KATIBA:

a) Marekebisho au masahihisho ya Katiba hii yanaweza kufanyika kwenye Mkutano Mkuu (General Conference) kwa kura ya maoni ya theruthi mbili (2/3) ya wajumbe wa Mkutano Mkuu endapo sahihisho/rekebisho hilo lilipelekwa kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu (General Conference) miezi mitatu (3) kabla ya siku ya mkutano.

b) Kanisa la Evangelistic Assemblies of God Tanzania litasajiliwa serikalini kwa mujibu wa sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Uandikishaji wa vyama Cap. 337.

c) Ili kuendeleza moyo wa Kikisto na kuendeleza kulinda misingi yake "The Evangelistic Assemblies of God Tanzania" itasimamiwa na kuongozwa na katiba hii, na sahihisho/rekebisho lolote litakalofanywa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa theluthi mbili za siri za kuandika itabidi liwasilishwe kwa Msajili wa vyama kama sehemu ya katiba hii.

**INATHIBITISHWA KUWA HII NI NAKALA HALISI YA KATIBA YA "THE EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA"**

**Signature (Trustees-EAGT)**



nfinix HOT 30i

CamScanner

ASSEMBLIES OF GOD

EAGT

CamScanner